

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb.Na. AC.40/135/01/7

13/11/2025

**TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA YA
HALMASHAURI YA WILAYA YA NSIMBO.**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo anawatangazia wananchi wote wenye sifa za kuomba nafasi ya Mwenyekiti wa

A. SIFA ZA MWOMBAJI.

1. Awe Raia wa Tanzania, Mkazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo mwenye umri kuanzia miaka 55 hadi 65.
2. Awe mwadilifu
3. Awe na ufahamu katika mojawapo ya fani zifuatazo:-
 - Menejimenti ya Rasilimali watu (Human Resources Management).
 - Utawala wa Umma (Public Administration).
 - Sheria (Law).
4. Awe Mstaafu Serikalini.
5. Awe hajawahi kushtakiwa kwa kosa lolote la Jinai.

B. KAZI ZA MWENYEKITI WA BODI YA AJIRA.

1. Kuendesha/Kuongoza vikao vya Usahili wa waombaji wa nafasi za kazi.
2. Kuendesha/Kuongoza vikao vya kuthibitisha kazini Watumishi
3. Kuendesha/Kuongoza vikao vya kupandisha/Kuwabathibitisha watumishi vyeo.

C. POSHO.

Kazi hii haina Mshahara wa kila mwezi. Mwenyekiti wa Bodi ya ajira atakuwa analipwa posho kutokana na vikao vitakavyokaliwa na Bodi.

D. MAELEKEZO:

1. Waombaji wote watume barua za maombi zikiwa na viambatisho vifuatavyo:-
 - (i) Cheti cha kuzaliwa.
 - (ii) Vivuli vya vyeti vya masomo na Taaluma (Certified)
 - (iii) Barua ya utambulisho toka kwa Mwenyekiti wa Kijiji.
 - (iv) Picha 2 za pasipoti za hivi karibuni.
 - (v) Wasifu binafsi (CV).
2. Barua toka kwa wadhamini wawili (02) zikiwa na anuani kamili.
3. Maombi haya yatumwe kuanzia tarehe 14/11/2025 hadi tarehe 28/11/2025.
4. Barua zote za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo,
S.L.P 688,
MPANDA.



Christina D. Bunini

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

NSIMBO.

**MKURUGENZI MTENDAJI CW
NSIMBO.**

Nakala: Katibu Tawala (M)

S.L.P 235,

MPANDA - KATAVI,